



## **TANGAZO LA KUAHIRISHWA KWA USAILI WA CHUO KIKUU CHA DAR ES SALAAM**

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawataarifu waombaji kazi wa nafasi mbalimbali waliokuwa wameitwa kwenye usaili kuanzia tarehe 19 Machi 2020 hadi 27 Machi 2020 kuwa usaili umeahirishwa mpaka watakapofahamishwa tena. Hii ni kutokana na kuepusha uwezekano wa kuendelea kusambaa kwa ugonjwa wa virusi vya CORONA.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinawaomba radhi waombaji wote wa kazi kwa usumbufu utakaojitokeza kutokana na kuahirishwa kwa usaili.

Imetolewa na:

Ofisi ya Naibu Makamu Mkuu wa Chuo – Utawala  
**Chuo Kikuu cha Dar es Salaam**  
18 Machi 2020